(102)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Modeco A,
S.L.P 845,
67115 MOROGORO
Simu: 0738 150 143
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

Morogoro Agosti 11, 2023.

TAKUKURU MOROGORO YASHIRIKISHA WADAU KATIKA UTATUZI WA KERO.

Ndugu WanaHabari,

Kupitia programu ya TAKUKURU Rafiki iliyozinduliwa na kuanza utekelezaji wake mwezi Februari 2023 imeweza kuwafikia wananchi wanaoishi katika kata zaidi za 36 za Mkoa wa Morogoro.

Lengo la programu hii ni kuibua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi katika maeneo yao ili ziweze kujadiliwa na kutatuliwa na wahusika kwa wakati.

Aidha kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni 2023, kupitia program ya TAKUKURU RAFIKI yafuatayo yamefanyika;

Kwanza, Programu hii imeweza kuongeza uelewa wa wananchi kwa kuwajengea ujasiri wa kuibua na kutoa kero mbalimbali ambazo kama zingeachwa zingeweza kupelekea vitendo vya rushwa kushamiri.

Pili, imewezesha kujenga na kuimarisha mahusiano mazuri kati ya TAKUKURU na watoa huduma wa taasisi mbalimbali katika utatuzi wa kero zilizowasilisha kwao na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Tatu, Kuongeza dhana ya uwajibikaji katika utumishi wa umma hasa katika kuhakikisha huduma zinazotolewa na taasisi husika zinatelekezwa kwa

fanisi. Aidha wasimamizi wa miradi ya maendeleo katika maeneo inayotekeleza Miradi hiyo, wameweza kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

Ndugu WanaHabari

Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika kipindi cha Mwezi **Aprili** hadi **Juni 2023,** tulifanikiwa kufuatilia jumla ya Miradi ya Maendeleo 07 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita na Thelethini na Sita, Mia Nne Themanini na Nane Elfu, Mia Saba Hamsini na Tano [1,636,488,755]. Katika ufuatiliaji tuliofanya tulibaini kasoro kadhaa** (Kiambatisho 1)

Ndugu WanaHabari

Uchambuzi wa Mifumo

Katika kipindi cha **Aprili 2023** hadi **Juni 2023** TAKUKURU Mkoa wa Morogoro tumefanya chambuzi za mifumo **kumi na mbili (12)**

- katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero tumefanya uchambuzi wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa mapato yatokanayo na ushuru wa madini ujenzi kijiji cha signal, Warsha/ Kikao na wadau kujadili na kuweka mkakati wa kuziba mianya ya rushwa katika usimamizi wa mapato yatokanayo na ushuru wa madini ujenzi kijiji cha signal, Warsha/ Kikao na wadau kujadili na kuweka mkakati wa kuziba mianya ya rushwa katika ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Ifakara, Ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio katika kuziba mianya ya rushwa katika ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Ifakara.
- Katika Manispaa ya Morogoro Mjini tumefanya uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa utoaji mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

- Katika halmashauri ya Wilaya Ulanga tumechambua wa mfumo kuhusu usimamizi wa mazao ya misitu, Uchambuzi wa mfumo katika ununuzi na upatikaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya na Jumuiya ya wasambazaji maji wa kata ya Vigoe.

- Katika halmashauri ya Wilaya Mvomero tumefanya uchambuzi wa mfumo wa matumizi ya asilimia 10 ya Mapato ya ndani ya halmashauri ya

Mvomero kwa ajili ya makundi maalumu (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu), Uchambuzi wa mfumo wa mianya ya Rushwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa mfumo wa "Force account", Uchambuzi wa mfumo wa utekelezaji wa maazimio ya Udhibiti wa Mianya ya Rushwa katika utendaaji kazi wa ASASI ZA KIRAIA (**AZAKI**) Nchini. **(Kiambatisho 2)**

Ndugu WanaHabari
Utekelezaji wa TAKUKURU RAFIKI

Katika kutekeleza programu ya TAKUKURU Rafiki, ofisi ya TAKUKURU (M) Morogoro kwa kushirikiana na wadau kutoka kwenye sekta mbalimbali imeweza kuzifikia kata 24 na kuibua kero 278 na kero 141 zilitatuliwa **(Kiambatisho 3)**

Ndugu WanaHabari
Uchunguzi na Mashtaka

Katika kipindi cha Mwezi Aprili 2023 hadi Juni 2023, tulipokea jumla ya taarifa **92** na kati ya hizo, taarifa **62** zinahusiana na vitendo vya rushwa na uchunguzi wake uko katika hatua mbalimbali ambapo taarifa **30** hazikuhusiana na vitendo vya rushwa na kwamba watoa taarifa hao walishauriwa jinsi ya kufuatilia malalamiko yao pamoja na kuwatatulia kero zao kwa kuwapeleka kwenye mamlaka husika.

Aidha, sekta zilizolalamikiwa ni kama ifuatavyo: **Taasisi za Fedha na Mikopo** (14), **Tamisemi/ Watendaji wa Mitaa/Vijiji na Kata** (10), **Polisi** (09), **Ardhi** (09), **Elimu** (09), **Mahakama** (07), **Afya** (05), **Binafsi** (03), **Tawa** (03), **Usafirishaji** (02), **Kilimo** (02), **Maliasili** (02), **Baraza la Ardhi** (02), **Mifugo** (02), **Sekta binafsi** (01), **Ajira** (02), **Mifuko ya hifadhi ya jamii** (01), **Jeshi la akiba** (01), **Tarura** (01), **Baraza la Ushuluhishi** (01), **Michezo** (01), **Nida** (01), **Utawala** (01), na **Tanesco** (01).

Kesi Mpya	Kesi zilizoamuliwa	Kesi zilizoshinda	Kesi zilizoshindwa	Kesi zilizoondolewa	Kesi zinazoendelea Mahakamani
07	06	01	02	03	10

Ndugu WanaHabari,
Elimu kwa Umma

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili **2023** hadi **Juni 2023**, kupitia Dawati la Elimu kwa Umma, tumeweza kufanya jumla ya Mikutano ya Hadhara **Kumi na Tano (15),** tumefanya **semina** kwa wananchi, watumishi wa umma na wa sekta binafsi **Thelathini na Tisa (39),** tumeimarisha klabu za wapinga rushwa wa shule za msingi, sekondari na vyuo **Arobaini na Tano (45),** tumeandaa na kurusha vipindi vya Redio na TV **Nane (08),** Tumeshiriki katika maonesho **Kumi na Mbili (12),** Uandishi wa Makala **Nane (08)** pamoja na utoaji wa habari kwa umma kupitia vyombo vya habari **Moja (01).**

Ndugu WanaHabari
Yatokanayo na Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023
Mnamo tarehe 06/05/2023 hadi tarehe 14/05/2023 ~~mbio za~~ Mwenge wa Uhuru 2023 ulikimbizwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Morogoro na kukagua miradi ya maendeleo. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi iliyokuwa na mapungufu ni kama ifuatayo ambapo TAKUKURU iliichunguza na kubainisha matokeo hatua zilizochukuliwa.

Halmashauri	Mradi	Kilichobainika	Hatua iliyochukuliwa
Halmashauri ya Wilaya Morogoro	Ujenzi wa vyumba **Vinne (4)** vya Madarasa katika shule ya Sekondari Fulwe wenye thamani ya **Tsh 80 Milioni**	➢ Kutokuwepo kwa nyaraka za mradi wakati wa ujio wa mwenge. ➢ Kutokujaza kwa usahihi	➢ Uchunguzi ulifanyika na kubaini kuwa baadhi vifaa vilivyobaki vilikuwa vimehamishiwa katika mradi mwingine, na taratibu za uhamishaji wa vifaa hivyo zilifuatwa isipokuwa nyaraka kuhusiana na uhamishaji wa vifaa hazikuwasilishwa kwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 kwa ajili ya ukagauzi. ➢ Aidha kulikuwa na mapungufu katika ujazaji wa vitabu (store ledger)

		wa vitabu vya stoo [store ledger]	kutokana na uelewa mdogo wa wahusika. ➢ Mkurugenzi wa H/Wilaya ya Morogoro alishauriwa kutoa elimu kuhusu usimamizi wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujazaji na utunzaji wa nyaraka muhimu kuhisiana na miradi.
Halmashauri ya Wilaya Gairo	Ujenzi wa barabara ya Unguu – Sabato yenye thamani ya Tsh **299.9 Milioni**	Thamani ya fedha hailingani na ujenzi wa mradi. Taratibu za kubadilisha ujenzi wa mradi kutoka Barabara ya lami Kwenda Barabara ya zege/mawe hazikuzingatiwa.	Uchunguzi wa awali ulifanyika na kubaini kuwa, taratibu za kubadilisha mradi kutoka ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami hadi kiwango cha mawe/zege zilifuatwa ambapo mabadiliko hayo yalifanywa na ngazi ya TARURA Mkoa. Kilichokosekana ni nyaraka katika eneo la mradi wakati wa mbio za Mwenge. Aidha thamani ya mradi inalingana na kiasi cha fedha kilichotumika

Ndugu WanaHabari

Mikakati ya vipaumbele kwa kipindi cha Julai 2023 – Septemba 2023

Katika kipindi tajwa tumejiwekea mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuchunguza taarifa zilizoibainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa lengo la kuthibitisha tuhuma, ili wahusika

waweze kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na ubadhirifu uliofanyika katika maeneo yao ya kazi.

Pili, tunaendelea kufuatilia fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na Serikali ili ziweze kutumika kutokana na malengo yaliyokusudiwa. Aidha niwakumbushe wananchi waweze kufahamu na kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao na pindi wanapobaini ubadhirifu wowote waweze kutoa taarifa TAKUKURU ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Tatu, tunaendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa jamii kupitia mikutano ya hadhara, semina, maonesho na vyombo vya habari. Tunaamini elimu hii ikitolewa kwa kiwango kikubwa itasaidia kudhibiti vitendo vya rushwa vinavyojitokeza katika utekelezaji wa majukumu.

Nitoe rai kwa wananchi kushirikiana na TAKUKURU katika kuvitokomeza vitendo vya rushwa kwa ajili ya kulinda maadili ya taifa letu.

Nne, tunaendelea na utekelezaji wa programu ya **TAKUKURU RAFIKI** kwa kufikia kata ambazo bado hazijafikiwa kwa ajili ya kubainisha kero mbalimbali zinazowakabili wananchi na kuzitafutia ufumbuzi kwa kuwekeana mikakati na wahusika.

Tano, Kufuatilia fedha za mikopo ya asilimia kumi [10%] zilizotolewa na Halmashauri kwa ajili kuwezesha vikundi kujiinua kiuchumi. Zipo taarifa kwamba sehemu kubwa ya vikundi vilivyokopeshwa kupitia mpango huo, vimeshindwa kufanya marejesho kwa wakati kitu ambacho kinakwamisha vikundi vingine kupata mkopo. Hivyo tunatoa rai kwa vikundi vyote ambavyo havijafanya marejesho vihakikishe vinarejesha mapema iwezekanavyo kabla havijachukuliwa hatua za kisheria.

Ndugu WanaHabari

Ifahamike kuwa jukumu la kuzuia na kupambana na Rushwa ni la kila mmoja wetu kupitia kauli mbiu ya KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU TUTIMIZE WAJIBU WETU, hivyo hatuna budi wote kwa pamoja

nasipo kujali itikadi za vyama, dini, mila, rangi wala kabila kushirikiana katika kudhibiti vitendo vya rushwa. Tunaamini kuwa kwa umoja huo tunaweza kuitokomeza rushwa nchini.

Ndugu WanaHabari,

Ninatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kufika katika ofisi zetu ambazo ziko kila wilaya au kwa kupiga simu ya bure **113**, ujumbe mfupi wa maandishi ***113#** au kupiga simu kwa Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro namba **0738150143** na Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro Namba **0754 834622.**

Aidha wananchi waliopo Wilayani wanaweza kuwasiliana na Wakuu wa TAKUKURU Wilaya kwa namba zifuatazo: - Kilombero **0738 150 145,** Kilosa **0738 150 146;** Mvomero **0738 150 147**, Ulanga **0738 150 148;** Malinyi **0738150149** na Gairo **0767 531 177.**

Vile vile niwaombe wananchi wawe tayari kutoa ushirikiano pindi watakapohitajika kwa ajili ya ushahidi Mahakamani.

....Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza...

Imetolewa na:-

Manyama Tungaraza,
Mkuu wa TAKUKURU Mkoa
MOROGORO
Simu ya Mkononi: 0738 150 143
Baruapepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz

KIAMBATISHO 1

Na.	Aina ya Mradi	Thamani ya mradi [TSH)	Kilichobainika	Hatua iliyochukuliwa
01.	**Halmashauri ya Wilaya Kilombero** Ufuatiliaji wa ujenzi wa mradi wa kalvati 3, ukarabati wa barabara Mkamba hadi Kiwandani na Kisawasawa hadi Mpanga -	152,485,000	Kalvati moja bado halijajengwa. Barabara ya Kisawasawa hadi Mpanga haijakarabatiwa kutokana na mvua kubwa zilozokuwa zikiendelea kunyesha.	Mkandarasi ameagizwa kurudi eneo la mradi kukamilisha kazi yake baada ya mvua kukatika.
02.	**Manispaa ya Morogoro** Ukaratabati wa barabara za mjini-	687,376,895	Kuongezeka kwa kazi tofauti na makubaliano ya mkataba wa awali.	Walishauriwa kufuata taratibu za mikataba pamoja na utunzaji wa nyaraka.
03.	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Matengenezo ya muda maalum, sehemu korofi na ujenzi wa kalvati barabara za tarafa ya Vigoi,	152,522,000	➢ Baadhi ya kalvati kushindwa kupitisha maji ➢ Baadhi ya sehemu za barabara kutokushindiliwa vizurii	Mkandarasi aliagizwa kufanya marekebisho sehemu zilizokuwa na dosari
04.	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Ukarabati wa barabara ya Makanga-Mafinji 10km,	560,204,860	➢ Baadhi ya kalvati kushindwa kupitisha maji ➢ Baadhi ya sehemu za barabara kutokushindiliwa vizuri ➢ Kubomoka kwa kalvati zilizokwisha	Mkandarasi aliagizwa kufanya marekebisho sehemu zilizokuwa na dosari

			kujengwa kabla ya mradi kukamilika ➢ Kukosekana kwa alama za barabarani	
05	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Ukarabati wa kituo cha walimu (TRC)-vigoi,	22,000,000	➢ Ufanisi hafifu katika kupiga chupping kwenye madirisha. ➢ Uchelewashaji wa samani (meza na viti).	➢ Msimamzi wa mradi alishauriwa kusimamizi mradi pamoja kutekeleza mapungufu yaliyobaini
06	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Ukamilishaji wa chumba kimoja cha darasa shule ya msingi Ikungua,	12,500,000	Udhaifu katika Utunzaji wa kumbukumbu za mradi	Halmashauri imeshauriwa kutoa elimu kuhusu utunzaji wa kumbukumbu za mradi.
07	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 3 ya vyoo shule ya msingi Msogezi,	49,400,000	➢ Kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi ➢ Ubora usioridhisha wa tofali ➢ Udhaifu katika utunzaji wa kumbukumbu za nyaraka za mradi	➢ Maelezo yametolewa kuhusu utekelezaji wa mradi kulingana muda uliyowekwa ➢ Halmashauri imeshauriwa kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu za nyaraka za mradi kwa wahusika.

KIAMBATANISHO 2

Na.	Uchambuzi	Kilichobainika	Hatua iliyochukuliwa
01.	**Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero** Uchambuzi wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa mapato yatokanayo na ushuru wa madini ujenzi kijiji cha signal-	➢ Kutofautiana kwa kumbukumbu za tripu ya gari kati ya mkusanya ushuru eneo la machimbo na tripu za gari zilizopokelewa kwenye kampuni/wateja. ➢ Hakuna vizuizi katika barabara inayoelekea na kutoka eneo la machimbo. ➢ Kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi ya tripu za magari zilizofanyika kulingana na mapato yaliyokusanywa	Yalitolewa mapendekezo kuhusu namna ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika
02	**Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero** Warsha/ Kikao na wadau kujadili na kuweka mkakati wa kuziba mianya ya rushwa katika usimamizi wa mapato yatokanayo na ushuru wa madini ujenzi kijiji cha signal -	Maazimio 3 yaliwekwa; ➢ Uwekaji wa kumbukumbu tripu za magari ➢ utunzaji hafifu wa taarifa za mapato yanayotokana na tripu ➢ Kutokuweka vizuizi kwenye barabara zinazoelekea katika machimbo	➢ Kuongeza idadi ya wasimamizi katika machimbo. ➢ Wameweka dafatari kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na kutoa stakabadhi ➢ Kwa kushirikiana ana Halmashauri wanapewa muiongozo wa uwekaji wa vizuizi.
03	Warsha/ Kikao na wadau kujadili na kuweka mkakati wa kuziba mianya ya rushwa katika ujenzi wa Hospitali ya	➢ Matumizi kufanyika pasipo kufuata BOQ. ➢ Taratibu za manunuzi kutokuzingatiwa. ➢ Kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji.	➢ Kutolewa kwa elimu. ➢ Ufuatiliaji wa mapungufu yaliyojitokeza

	Halmashauri ya Mji Ifakara- **Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero**	➢ Kutokununuliwa kwa vifaa kwa wakati. ➢ Mradi Kutokukamilika kwa wakati. ➢ Kutokupatikana kwa baadhi za nyaraka.	
04	**Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero** Ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio katika kuziba mianya ya rushwa katika usimamizi wa mapato yatokanayo na ushuru wa madini ujenzi kijiji cha signal -	➢ Kutofautiana kwa kumbukumbu kati ya mkusanyaji ushuru na mteja ➢ Kutokuwepo kwa viuzizi katika barabara zinazotoka na kuelekea machimbo ➢ Kutokuwepo kwa kumbukumbu za tripu za magari	Ufuatiliaji unaendelea pamoja na kuwataka waweke kumbukumbu sahihi
04	**Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero** Ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio katika kuziba mianya ya rushwa katika ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Ifakara-	➢ Uzingatiaji wa taratibu za manunuzi ➢ Uzingatiaji wa Bill of Quantity (BOQ) ➢ Ushirikishwaji wa kamati mbalimbali ➢ Utunzaji wa kumbukumbu za nyaraka	Ufuatiliaji wa mapungufu yaliyojitokeza unaendelea
05	**Manispaa ya Morogoro Mjini** Uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa utoaji mikopo ya asilimia 10	➢ Mikopo kutolewa bila kufuata utaratibu ➢ Mikopo kutorejeshwa kwa wakati ➢ Mikopo kutolewa tofauti na malengo ya kikundi	TAKUKURU kusimamia urejeshwaji wa fedha za mikopo kwa vikundi ambavyo havijakamilisha madeni yao

	kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu-		
06	**Manispaa ya Morogoro Mjini** Uchambuzi wa mfumo wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa usimamizi wa miradi ya maendeleo kata ya Mkundi-	➢ Tathmini ifanyike pindi uchaguzi wa miradi inapofanyika. ➢ Ujenzi wa miradi ufanyike kulingana na BOQ ➢ Usimamizi wa miradi uzingatiwe ili miradi ikamilike kwa wakati.	TAKUKURU kusimamia utekelezaji wa miradi
07	Uchambuzi wa mfumo kuhusu usimamizi wa mazao ya misitu- **Halmashauri ya Wilaya Ulanga**	➢ Kutokuzingatiwa kwa taratibu za utolewaji wa leseni za uvunaji ➢ Udhaifu katika usimamizi wa leseni na vibali vinavyotolewa. ➢ Ushirikishwa hafifu katika mchakato wa upatikanaji wa wafanyabiashara wa mazao ya misitu	➢ Kuwaelimisha kuhusu uzingatiaji wa taratibu za utolewaji wa vibali na leseni za uvunaji
08	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Jumuiya ya wasambazaji maji wa kata ya Vigoe-	➢ Kutokuwepo kwa Uwiano kati ya mapato ya matumizi. ➢ Upotevu wa maji unaofanywa na wateja wa majumbani. ➢ Wanasiasa kuingilia majukumu ya jumuiya ya maji	➢ Kutoa elimu kwa viongozi wa kisiasa pamoja na wasimamizi
09	**Halmashauri ya Wilaya Ulanga** Uchambuzi wa mfumo katika ununuzi na upatikaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya -	➢ Kukosekana kwa muunganiko wa daktari aliyemtibu mgonjwa na Dirisha la utoaji la dawa. ➢ Kukosekana kwa mshitiri baada ya mkataba wa awali kuisha muda wake. ➢ Kutokuzingatia kumbukumbu za kupokea na utoaji wa	➢ Mganga mkuu wa Wilaya alishauriwa kuingia mkataba mpya na mshitiri ➢ Mganga Mkuu ameshauriwa kuhuisha mara kwa mara ili kujua kiasi cha dawa

		dawa.	kilichopo stoo na kilichoisha (Out stock)
10	**Halmashauri ya Wilaya Mvomero** Uchambuzi wa mfumo wa matumizi ya asilimia 10 ya Mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mvomero kwa ajili ya makundi maalumu (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu),	➢ Mfumo wa upokeaji wa fedha za marejesho ya mikopo hauruhusu kupokea sehemu ya rejesho la mwezi, isipokuwa rejesho kamili. Sharti hili huwafanya wakopaji kushindwa kufanya marejesho kwa wakati na matokeo yake wanashawishika kufanya matumizi mengine binafsi. ➢ Uchambuzi ulibaini kwa Mwaka 2022/2023 kati ya Fedha Tsh 164,900,000/= zilizokopeshwa kwa vikundi, zilirejeshwa Tsh 21,174,000/= ambayo ni sawa na asilimia 13 tu.	➢ Halmashauri imeshauriwa kuweka utaratibu wa kupokea marejesho ya fedha za mikopo hata kama kiasi hicho ni pungufu ya kiasi kinachotakiwa kurejeshwa. ➢ Halmashauri imeshauriwa kuunda timu ya kufuatilia urejeshaji wa mikopo
11	**Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.** Uchambuzi wa mfumo wa mianya ya Rushwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa mfumo wa "Force account" katika	➢ Kutoandaliwa kwa mipango ya manunuzi katika miradi inayotekelezwa kwa "**force account**" ➢ Kamati zinazoundwa za usamamizi wa miradi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kutekeleza majukumu yao.	➢ Halmashauri imeshauriwa kuandaa mipango ya manunuzi kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ya maendeleo. ➢ Halmashauri imeshauriwa kuelimisha Kamati za "force account" kuhusiana na wajibu walionao katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

1^	**Halmashauri ya Wilaya Mvomero** Uchambuzi wa mfumo wa utekelezaji wa maazimio ya Udhibiti wa Mianya ya Rushwa katika utendaaji kazi wa ASASI ZA KIRAIA (**AZAKI)** Nchini,	**AZAKI** nyingi hazikidhi matakwa ya serikali na miongozo ya uwasilishaji wa taarifa.	Halmashauri imeshauriwa kuhakikisha **kuwa AZAKI** zinazoanzishwa zinakidhi matakwa ya serikali na miongozo ya uwasilishaji wa taarifa

'IAMBATISHO 3

IDADI YA KATA ZILIZOFIKIWA	IDADI YA KERO ZILIZOTOLEWA	IDADI YA KERO ZILIZOTATULIWA	MIFANO YA KERO KISEKTA NA NAMNA ZILIVYOTATULIWA	MAFANIKIO YA TR KATIKA MKOA
24	278	141	1. Mikopo kausha damu inaumiza wanaokopeshwa. Maafisa wa kata/ Mtaa husika washirikishwe katika mikopo hiyo. **UTATUZI:** Elimu ya mikopo inaendelea kutolewa kwa wananchi kuhusu uzingatiaji wa masharti ya mikopo kabla ya kukopa. Aidha wananchi wanapaswa kufuatilia riba za mikopo kwenye taasisi mbalimbali kabla hawajachukua mikopo. 2. Umiliki wa ardhi ni gharama [bei za urasimishaji kuwa juu] **UTATUZI:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleoo ya Makazi ilitoa waraka kuhusu urasimishaji wa makazi kuwa zisizidi Tsh 250,000/= 3. Ubovu wa barabara ya Bigwa-Kisaki kutopitika kipindi cha masika. **UTATUZI:** Mkandarasi **M/s copex** anaendelea na ujenzi wa barabara tajwa yenye urefu wa Km. 109 4. Polisi kucheleweshwa kesi zinazohusu ukatili wa kijinsia na kutofikishwa Watuhumiwa	Kupitia programu ya TAKUKURU RAFIKI, Wananchi wanapata majibu ya kero zao kwa haraka sana na bila kutumia gharama zozote, kwani majibu ya kero zao yanatolewa katika vikao husika na pale ambapo wahusika hawapo katika vikao hivyo TAKUKURU ina wajibu wa kluwasilisha kero hizo katika idara Husika kwa ajili ya kupatiwa majibu na pale majibu yanapotolewa, TAKUKURU huwajibika kuwasilisha majibu hayo kwa wananchi husika.

			Mahakamani kwa wakati. **UTATUZI:** Polisi wanaendelea kutoa elimu kupitia Polisi Jamii kuhusu ukatili wa kijinsia kwa kuwataka wananchi kuwafichua wahalifu, utayari wa kutoa ushahidi Polisi, kutokuwa vigeugeu. 5. Mradi wa maji wa msererekо katika Kijiji cha Dalla Kata ya Mvuha kutokukamilika kwa wakati **UTATUZI:** RUWASA wanaendelea na usimamizi wa mradi ili uweze kukamilika na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama 6. Kutokuwepo gari la wagonjwa katika kituo cha afya Duthumi. **UTATUZI:** maombi yamewasilisha Gari la OR-Tamisemi kwa ajili ya gari la wagonjwa. 7. Kutokuwepo kwa huduma ya X-Ray katika kituo cha Afya Duthumi **UTATUZI:** Kituo cha afya Duthumi hakina jengo la X- ray hivyo haiwezi kuwepo. Aidha zimefanyika jitihada za kuwasilisha maombi OR-Tamisemi ili waweze kutenga fedha kwa ajili ya X- ray	Ushirikiano kutoka kwa wananchi na hasa kuhusiana na na utoaji wa taarifa za vitendo vya rushwa umeimarika. Uwajibikaji wa watumishi wa umma katika utowaji wa huduma umeongezeka.

			8. Upungufu wa dawa katika Zahanati ya Mvuha. **UTATUZI:** Zahanati ya Mvuha inazo dawa kulingana na mahitaji ya kituo. Aidha zahanati hiyo haiwezi kuwa na dawa zinazopatikana katika Hospitali ya Wilaya vituo vya Afya. Dawa wanazohitaji wananchi kwa kuwa wapo karibu na Hospitali ya Wilaya watazipata pale. 9. Kukosekana kwa uwazi katika uandikishaji majina ya wenye uihitaji katika umwagiliaji (Milola Scheme of irrigation- Ulanga. **UTATUZI:** wananchi wametangaziwa kuhusu uwepo wa uandikishaji kupitia mikutano ya hadhara iliyoitishwa na viongozi wa maeneo husika. 10. Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu taratibu za uunganishaji wa umeme majumbani- Ulanga **UTATUZI:** TANESCO wametoa elimu kwa wananchi kuhusu taratibu za uunganishaji wa umeme na pia wananchi wamefahamishwa kutowatumia vishoka katika kupata huduma ya umeme. 11. Vijiji havisomi mapato na matumizi kwa wakati na wakati	

			mwingine havisomi kabisa. **UTATUZI:** Kiliitishwa kikao kati ya Sekretalieti ya TAKUKURU RAFIKI na viongozi wa vijiji ili kuzungumzia changamoto ya kotosoma mapato na matumizi na kikao kiliazimia taarifa za mapato na matumizi zisome kwa wananchi. 12. Urasimu Tanesco kwenye zoezi la uwekaji na usambazaji wa Umeme, pia gharama zinazotozwa na TANESCO za kuingiziwa umeme ni kubwa sana. **UTATUZI: TANESCO** imeanzisha mfumo unaoitwa **NIKONEKT** mfumo huu unawawezesha wateja kuomba kuwekewa umeme kwa kutumia website ya TANESCO, mfumo huu utamsaidia mteja kupata huduma bila kufika ofisi ya TANESCO wala kumtafuta mfanyakazi amsaidie. **13.** Hakuna ushirikishwaji wa wananchi katika vikao vinavyohusu maji katika kata ya Turiani na TURUWASA. **UTATUZI:** Mamlaka ya Maji Turiani kuhudhuria vikao mbalimbali vya kata, na vijiji, pia imekuwa na utaratibu wa vikao vya kila robo mwaka na	

			Wadau kwa ajili ya kueleza utekelezwaji wa shughuli. 14. Watoa huduma ya Afya hawana lugha nzuri kwa wagonjwa katika Kituo cha Afya cha **MELELA** **UTATUZI:** Kamati kuitisha kikao na Viongozi wa Kituo cha Afya cha Melela na kuazimia kuwa viongozi wa Hospitali kuitisha Vikao na watumishi wote na wajumbe wa Kamati ya Kituo cha Afya Melela.	